

# USAIFIRI ARDHINI




■ Toleo la 1: Julai - Septemba 2022



**TUTUMIE TIKETI  
MTANDAO KWA  
MANUFAA YETU  
SOTE**

Uk9..

## Yaliyomo ndani...



Uthibitishaji wa Madereva ni  
Tija ya kuboresha Usalama na  
kupunguza Ajali za Barabarani  
Nchini

Uk 5



**Makongoro Nyerere  
ahimiza elimu, Tiketi  
Mtandao**

Uk 3



**LATRA kuongeza Ushirikiano  
Kiudhibiti kati ya Tanzania na  
Afrika Kusini**

Uk 4



# TAHARIRI

**K**aribu katika toleo la kwanza la Jarida la USAFIRI ARDHINI kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA). Jarida hili litakuwa likiandaliwa na kusambazwa mara nne kwa mwaka.

Katika jarida hili, utasoma na kujifunza kuhusiana na masuala kadha wa kadha yanayohusu huduma za usafiri ardhini nchini, ikiwa ni pamoja na kazi, majukumu na huduma za udhibiti wa usafiri ardhini.

Vilevile, kupitia jarida hili, utafahamu juhudhi na shughuli mbalimbali za utoaji wa elimu kwa umma ili kuwahabarisha wadau shughuli za mamlaka. Hii yote tunakuletea ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya usafiri ardhini.

Katika kipindi hiki, miongoni mwa mambo makubwa yaliyofanyika ni kuhamishia Makao Makuu ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) jijini Dodoma, kusajili na kuthibitisha madereva, kufanya mikutano ya kupanga nauli za treni, kuanza rasmi kwa matumizi ya tiketi mtandao, na azimio la kukomesha ukiukwaji wa masharti ya lese ni pamoja na Jeshi la Polisi.

Katika kuhamia Dodoma, imekuwa ni mafanikio kutekeleza agizo la Serikali lililozitaka taasisi za umma kuhamia Makao Makuu ya nchi yaliyopo jijini Dodoma. Kwa hiyo, wadau wote wa usafiri ardhini mnakaribishwa katika Ofisi za Makao Makuu ya LATRA yaliyopo Tambukareli, Dodoma. Kipekee kabisa nimshukuru kwa dhati Katibu Mkuu Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Bw. Gabriel

Migire kwa mapokezi mazuri na maelekezo aliyoyatoa ofisini kwake, Mji wa Mtumba, Jijini Dodoma.

Mamlaka imeendelea kutahini na kuthibitisha madereva ikiwa ni njia ya kuboresha uwezo wa madereva katika kudhibiti ajali zinazosababishwa

na makosa ya kibinadamu. Hivyo, natoa rai kwa madereva wanaoendesha vyombo nya moto kibiashara kutuma maombi katika mfumo wa kielektroniki wa kutahini madereva kupitia mfumo wa RRIMS unaopatikana kwa anwani ya <https://rrims.latra.go.tz>

Pamoja na hayo, mamlaka imeshiriki katika vikao mbalimbali vilivyofanyika Dar es Salaam, Arusha na Kigoma ili kujadili badiliko la bei za nauli ya treni. Mamlaka ilikutana na wadau mbalimbali ikiwemo Shirika la Reli Tanzania (TRC), na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC).

Katika jarida hili, utasoma makala ya Uthibitishaji Madereva na Tiketi Mtandao na utapata taarifa kwa kina kuhusu sababu za kuwathibitisha madereva pamoja na hali halisi ya utekelezaji wa tiketi mtandao nchini hadi kufikia mwezi Septemba mwaka huu. Si hayo tu, bali pia utasoma taarifa nyingine kadha wa kadha kuhusu sekta ya usafiri ardhini nchini.

Toleo hili ni mwanzo tu. Kutakuwa na mwendelezo wa matoleo mengine yanayofuata yatakayokupa taarifa za kina kuhusu maendeleo na udhibiti unaofanyika katika sekta ya usafiri ardhini nchini.

Mwisho kabisa, nitumie fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kufahamu vizuri maendeleo ya sekta ya usafiri ardhini na udhibiti wa huduma za usafiri ardhini,

Nakutakia usomaji mwema.



CPA Habibu J.S. Suluo



# KATIBU MKUU (UCHUKUZI) AWAPOKEA LATRA DODOMA

**K**atibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi anayeshughulikia Sekta ya Uchukuzi, Bw. Gabriel J. Migire Jumatatu tarehe 26 Aprili, 2022 aliwapeka baadhi ya watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhi-ni (LATRA) mara baada ya LATRA kutekeleza maelekezo ya Serikali kuhamishia rasmi makao yake makuu jijini Dodoma.

Akiongea na wajumbe wa menejimenti ya LATRA waliofika ofisi ni kwake, Bw. Migire aliwapongeza wafanyakazi na uongozi wa LATRA kwa kuweza kujipanga kufika Dodoma mapema kufuatia maelekezo ya Serikali yalivytangazwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jumatatu Septemba 5, 2022.

“Tunafahamu kuwa binadamu ni mzito kufanya mabadiliko, huenda baadhi yenu wakawa bado wanaona uzito katika hatua hii ya awali, napenda kuwashakikishia kuwa mtafurahia maisha ya Dodoma kwa kuwa Dodoma sasa ina fursa nyingi na kadri mnavyoishi huku mtazifahamu na kuzifurahia,” alisema

Aliongeza kuwa, ni muhimu LATRA kuongeza matumizi ya Serikali Mtandao ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali baada ya kuhamia Makao Makuu ya Nchi Dodoma.

Aidha alisema kuwa, ofisi yake iko tayari kutoa ushirikiano iwapo LATRA itakutana na changamoto zinazoweza



*Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi anayeshughulikia Sekta ya Uchukuzi, Gabriel J. Migire (katikati) akiwakaribisha wajumbe wa Menejimenti ya LATRA katika makao makuu ya LATRA, Dodoma*

kujitokeza katika siku za awali baada wakati.” alisema ya kuhamia Dodoma.

Kwa upanda wake, Mkurugenzi wa Dodoma, natoa shukrani kwa ush-Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo alisema kuwa LATRA ilijipanga kutekeleza maelekezo ya Serikali tanggu mapema na kuwa anawakaribisha irikano tuliuopata kwa Wizara kuititia Katibu Mkuu na viongozi wengine,” aliongeza

Aidha CPA Suluo ametoa shukrani wadau mbalimbali kufika ofisi za LATRA Makao Makuu zilizopo eneo la Tambukareli barabara ya Jakaya Kikwete jirani na Jengo la Mkandarasi jijini humo.

“Tangu nilipokabidhiwa ofisi tarehe 11 Julai, 2022 Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Gabriel Migire, alinipa maelekezo ya Serikali kuhusu kuhamia Dodoma, hivyo nilishirikiana na wenzangu tukafanya maandalizi yali-yotuwezesha kuhamia Dodoma kwa





# LATRA YATEKELEZA MIKAKATI KUBORESHAA USAFIGIRI WA RELI NCHINI

**M**kurugenzi Mkuu wa Mam-laka ya Udhibiti Usafiri Ar-dhini (LATRA), CPA Habibu J. Suluo amesema kuwa LATRA imejipanga kuimarisha huduma za udhibiti usafiri ardhini nchini ikiwemo usafiri wa reli ili kufikia azma ya Serikali ya kuweze-sha usafiri bora na salama kote nchini.

Ameyasema hayo jijini Dodoma al-ipokuwa akifungua mafunzo yanayotolewa kwa wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) wanaoshughulika na uendeshaji wa treni moja kwa moja yaliyoandaliwa na LATRA kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Mafunzo hayo yaliyofanyika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Kigoma, Tabora na Morogoro na ku-wafikia wafanyakazi zaidi ya 150 kuto-ka mikoa yenye usafiri wa reli nchini.

Aliungeza kuwa LATRA imeongeza mikakati ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wanaoshughulika na uendeshaji wa treni moja kwa moja kwa kuwasilimaliwatu ni wasilimali muhimu na ghali zaidi. Watu wanaweza kuongeza au kupunguza ufanisi wa shirika la reli kulinganga na jinsi wanavyotekeleza kazi zao.

“Zaidi ya asilimia 90 ya ajali za treni zinasababishwa na makosa ya kibinada-mu, hii inatokana na kutozingatia miongozo yetu katika utendaji. Ninawasihi, kila mmoja azingatie mafunzo haya na akayafanyie kazi ip-asavyo. Ajali ni kiashiria kikubwa cha

upungufu katika uendeshaji wa treni zetu. Ajali hizi zinaleta hasara kubwa kwa kupoteza maisha ya watu, ku-haribu miundombinu ya reli na mali,” alisema.

Aidha, CPA Suluo alisisitiza kuwa, ajali inapotokea, kila mmoja ajitath-min iwapo alitimiza wajibu wake ipasavyo. Ikitokea watu wamepote-

na kuacha huduma zetu zikiendeshwa kwa hasara,” alifafanua.

Kwa upande wake, Kaimu Mku-rugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Reli, Mhandisi Hanya Mbawala alisema kuwa baada ya mafunzo hayo kuka-milika, itafanyika tathmini ya kuju-matokeo na mapokeo ya mafunzo haya ambayo baadaye yatafanywa kwa yali-



za maisha kwa sababu mmoja wetu hakutimiza wajibu wake, mtu huyo anakuwa ametenda makosa makubwa kwa mujibu wa miongozo ya utendaji kazi na ni dhambi kubwa hata katika imani yake.

“Reli zetu zinategemewa sana katika usafirishaji ndani na nje ya nchi ikiwemo nchi ambazo hazifikiwi na bahari. Huduma zetu ni lazima ziwe shindani kwa kuwa wateja wana uwezo wa kutumia huduma mbadala

yopangwa kufanyika kwa ngazi zote za watendaji wa TRC.

“Wafanyakazi hawa ni muhimu sana kwa kuwa ndiyo wanaofanya TRC ite-keleze kazi zake ipasavyo. Baada ya mafunzo kwa ngazi hii ya watendaji wa moja kwa moja, tutawafanyia ma-funzo ngazi ya menejimenti na hati-maye Bodi ya Wakurugenzi, ili kuhaki-kisha kunakuwa na uelewa wa pamoja katika kuboresha huduma za usafiri wa reli nchini ikiwemo reli ya kisasa in-ayotarajiwa kuanza kufanya kazi hapo baadaye,” alisema Mhandisi Hanya.

**Zaidi ya sili-mia 90 ya ajali za treni zinasababishwa na makosa ya kibinadamu**



# MAKONGORO NYERERE AHIMIZA ELIMU, TIKETI MTANDAO

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mhe. Makongoro Nyerere ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuendeleza matumizi ya teknolojia katika udhibiti wa huduma za usafiri ardhini ikiwa ni pamoja na matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao ili kuongeza tija kwa wasafirishaji, abiria na Serikali kwa ujumla.

Ameyasema hayo tarehe 14 Septemba, 2022 katika kikao chake na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA Habibu J. Suluo kilichofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara mjini Babati. Kikao hicho kilichohudhuriwa na Katibu Tawala Mkoa wa Manyara, Bi. Caroline Mthapula na baadhi ya maofisa wa LATRA ikiwa ni sehemu ya ziara ya Mkurugenzi Mkuu wa LATRA mkoani humo.

‘Nilipata bahati ya kujifunza zaidi kuhusu mfumo huu ambao nilikuwa nikiusikia, baada ya kukaa na wataalamu, nimegundua kuwa mfumo wa Tiketi Mtandao unamsaidia mmiliki wa basi kukusanya mapato yake kwa ufanisi zaidi, unamrahisishia abiria kununua tiketi kwa urahisi na una saidia Serikali kukusanya mapato kwa ufanisi’ alisema Mhe. Makongoro.

Aliungeza kuwa mfumo huo una saidia kudhibiti upandishaji holela wa nauli kipindi cha mahitaji makubwa ya huduma ikiwemo kipindi cha sikuu za mwisho wa mwaka.

Aidha, Mheshimiwa Nyerere emeia giza LATRA kuongeza utoaji wa elimu na kuwafikia wadau wengi zaidi kwa kuwa matumizi ya teknolojia ndiyo

muafaka wa kuleta mapinduzi katika sekta ya usafiri nchini.

‘Tunakoelekea ni abiria kuweza kujihudumia mwenyewe bila kutegemea kuhudumiwa na mtu, labda mizigo ndiyo itahitaji kuhudumiwa, kwa kuwa Tanzania ni sehemu ya dunia, maendeleo hayo hatuwezi kuyaepuka,’ alisema.

Amesema kuwa ofisi yake itaendelea kushirikiana na LATRA ambapo

ameahidi kufanya kazi maelekezo ya mkuu huyo wa mkoa na kuendeleza ushirikiano na elimu kwa wadau wote ili Serikali ifikie malengo yake kwa wakati.

Katika ziara yake mkoani Manyara, CPA Suluo alipata fursa ya kutembelea wadau mbalimbali wakiwemo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, ACP George Katabazi na Kaimu Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa



*Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mhe. Makongoro Nyerere (kulia) akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo(kushoto) baada ya kikao kilichofanyika katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa Manyara*

ameiagiza LATRA kuendeleza ushirikiano na wadau wote wakiwemo Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na wasafirishaji ili kuongeza tija katika sekta ya usafirishaji ambayo inatoa ajira nyingi kwa wananchi na kusaidia kufikia malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoonozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wake, CPA Suluo

wa Manyara, ASP Mahenda Kera ambapo walipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali ya ushirikiano ikiwemo utekelezaji wa matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao.





# LATRA YAENDELEA KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ZA TEKSI MTANDAO

**M**kurugenzi Mkuu LATRA CPA Habibu Suluo amesema kuwa Mamlaka inaendelea kushughulikia changamoto za huduma za teksi mtandao, ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na madereva na kampuni za teksi mtandao nchini.

CPA Suluo amesema hayo Septemba 12, 2022 jijini Arusha alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu Mkutano wa Wadau wa Reli, Tiketi Mtandao na Mazungumzo kuhusu Tiketi Mtandao.

Aidha ameeleza kuwa, kati ya tarehe 5 na 8 Septemba, 2022, Mamlaka ilifanya vikao na Chama cha Madereva wa Teksi Mtandao Tanzania (TODA), kampuni za Bolt na Uber ili kubadilishana taarifa na hoja za kibashara na kiuchumi ili kusaidia kampuni za mifumo ya teksi mtandao, madereva na abiria kupata huduma bora, endelevu na kwa thamani halisi ya pesa.

CPA Suluo ameongeza kuwa, “kufuatia vikao hivyo, Mamlaka imeona itoe taarifa kwa umma kwamba vikao vyetu na mazungumzo yetu na TODA, Bolt na Uber yalikwenda vizuri. Kuna taarifa ya maandishi tunasubiri tupate leo na si zaidi ya kesho toka kwa Bolt na Uber ili na sisi tukamilishe taratibu zetu za ndani kabla hatujatangaza rasmi maamuzi ya Mamlaka.”

“Niwashukuru kipekee Uongozi wa TODA na watoa huduma wa teksi mtandao walioendelea kutoa huduma ikiwa ni pamoja na Paisha, Ping, In-drive na Little Ride,” amesema CPA Suluo.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini mtandao za Bolt na Ubber zilisitisha (LATRA), kwa mujibu wa Sheria Na. baadhi ya huduma za usafiri wa teksi 3 ya mwaka 2019 ilitangaza viwan- mtandao kufuatia kutoridhika na kigo vya nauli za teksi mtandao kupitia Gazeti la Serikali Na. 1369 la tarehe wango cha ukomo cha kamisheni cha 8 Aprili, 2022 na vyombo vingine vya madereva husika. habari. Kampuni za mifumo ya teksi

## LATRA KUONGEZA USHIRIKIANO KIUDHIBITI KATI YA TANZANIA NA AFRIKA KUSINI



*Wajumbe wa Menejimenti wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo pamoja na Wataalamu kutoka Taasisi ya Serikali ya Afrika Kusini inayosimamia masuala ya Usafirishaji Nje ya Mipaka*

**M**amlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendesha kikao kazi na wataalamu kutoka Taasisi ya Serikali ya Afrika Kusini inayosimamia masuala ya Usafirishaji Nje ya Mipaka (Cross Border Road Transport Agency (C-BRTA) - South Africa) katika makao makuu ya LATRA Dar es Salaam kwa lengo la kujadili na kujifunza namna shughuli za udhibiti usafiri ardhini zinavyotekeliza nchini.

Akizungumza katika ufunguzi wa kikao kazi hicho, Mkurugenzi Mkuu LATRA, CPA Habibu Suluo amesema

kikao hicho kitaongeza ushirikiano uliokuwepo baina ya nchi hizo mbili.

“Ushirikiano kati ya nchi hizi mbi- li umekuwapo kwa muda mrefu, nadhani mnapajua Morogoro ambapo ndipo Mashujaa wa Afrika Kusini waliweka kambi. Hivyo kikao kazi hiki kitaongeza na kudumisha ushirikiano uliokuwapo kiuchumi, kijamii, kisiasa na hata kiutamaduni,” amesema CPA Suluo.

Naye Meneja Mipango na Udhibiti kutoka C-BRTA Afrika Kusini, Wakili Khatu Mafuraha ambaye pia ni Mkuu wa msafara huo, ameishukuru LATRA



# UTHIBITISHAJI WA MADEREVA NI TIJA YA KUBORESHA USALAMA NA KUPUNGUZA AJALI ZA BARABARANI NCHINI

Ulishawahi kuijuliza ni madhara gani yanatokana na ajali za barabarani au taabu wanazopitia waathirika wa ajali? Na je, vipi kuhusu familia zinazobaki baada ya kupoteza wapendwa wao kama athari za ajali hizo?


Watu wengi hupitia wakati mgumu na kushindwa kuendelea na shughuli zao za kila siku kutokana na athari za moja kwa moja zinazotokana na ajali za barabarani mathalani kuwa majeruhi, kupata ulemavu wa maisha au hata kupoteza maisha.

Athari hazipo tu kwa abiria wanaotumia vyombo hivyo vya usafiri pindi wanapopata ajali, bali kwa wamiliki wa vyombo pia hupata hasara kwa kuharibikiwa vyombo vya usafiri, Serikali hupata hasara kwa uharibifu wa miundombinu ya barabara na kuingia ghamama za kufanya matengenezo.

Mzigo huu hubebwa nasi sote kama taifa tunapolazimika kutumia fedha za kigeni kununua magari mapya kama mbadala wa magari yaliyopata ajali, kununua vipuri na madawa kwa ajili ya kutibia majeruhi wa ajali hizo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi kuhusu Takwimu ya Hali ya Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani ya mwaka 2020, asilimia 91.6 ya ajali zinazotokea Tanzania Bara zinatokana na uzembe na makosa ya kibinadamu kama vile uendeshaji wa hatari, uzembe wa watumiaji wa barabara, mwendokasi na ulevi.

Takwimu hizo zinaonesha vyanzo vingine vya ajali kuwa ni asilimia 5.7 inayochangiwa na ubovu wa vyombo vya moto na asilimia 2.7 inayochangiwa na sababu za kimazingira kama vile



*Takwimu ya Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ikioneshwa hali ya vyanzo vya ajali za barabarani kwa mwaka 2020*

moto, vizuizi vya njia pamoja na ub- kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ovu wa barabara. ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA)

Hali hii imekuwepo kwa muda mre- fu na kupelekeea Serikali ya Jamhuri ya LATRA imepewa jukumu la kuthibit- Muungano wa Tanzania ambapo mwa- isha madereva na kusajili wahudumu ka 2019 Serikali iliipatia Mamlaka wanaotoa huduma za usafiri kibiashara ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kama vile daladala, mabasi ya masafa jukumu la kuthibitisha madereva na marefu, malori, na kadhalika. kusajili wahudumu wa magari ya bi-

ashara.

LATRA inatekeleza jukumu hilo sha usalama katika sekta zinazodhibi- kwa kuchukua hatua za ziada na kuan- tiwa ambazo ni sekta za usafiri wa zisha mfumo wa kutahini madereva barabara, usafiri wa reli na usafiri wa (Drivers Testing System - DTS) ili waya (cable transport).

kupima maarifa ya madereva wenye Aidha, Bi. Mloge anaongeza kuwa, leseni za kuendesha magari ya biasha- ili kufanikisha utaratibu wa kusajili na ra. Hatua hii inalenga kusaidia kupun- kuwathibitisha madereva na wahudu- guza ajali za barabarani na kuhakikisha mu, LATRA iliandaa kanuni zinazofa- usalama kwa watumiaji wa huduma za hamika kama Kanuni za Kuthibitisha usafiri wa barabara.

Akuelezea mfumo wa DTS kishe- Vyombo vya Moto Vinavyofanya Kazi ria, Mkoo wa Kitengo cha Sheria LA- Kibiashara ambazo zilitangazwa kat- TRA, Bi. Selina Mloge anasema kuwa, ka Gazeti la Serikali Na. 81 la tarehe 7

**Inaendelea UK 7**



## UTHIBITISHAJI WA MADEREVA NI TIJA YA KUBORESHA.....

**Inatoka Uk 6**

Januari, 2020.

Akizungumzia namna dereva anavyoweza kuthibitishwa, Bi Mloge anasema kuwa, kwa mujibu wa Kanuni za Kuthibitisha Madereva na Kusajili Wahudumu wa Vyombo vya Moto Vinavyofanya Kazi Kibiashara, 2020, Kanuni ya (4)(1) inamtaka kila dereva anayeendesha chombo cha moto kibiashara awe amethibitishwa na LATRA, kufanya kinyume chake ni kosa kisheria.

Vilevile Bi. Mloge anasema kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 22(2) dereva atakayeshindwa kukidhi masharti ya kanuni hizo anatenda kosa. Endapo atahukumiwa atapaswa kulipa faini ya kuanzia elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki mbili au kifungo kisichopungua miezi mitatu jela na kisichozi-di mwaka mmoja jela au vyote faini na kifungo.

Vilevile, alama zake (demerit points) zitapunguzwa kwa alama 10 kama ilivyoainishwa katika Jedwali la 5 Sehemu ya A kipengele cha 9 cha Kanuni za Kuthibitisha Madereva na Kusajili Wahudumu wa Vyombo vya Moto Vinavyofanya Kazi Kibiashara, (zilizofanyiwa Marekebisho) 2021.

Bi. Mloge anafanua kuwa, pale ambapo dereva atabainika kuendesha chombo cha moto kibiashara bila kuthibitishwa na mamlaka na kukiri kosa na kuomba kosa lake lififishwe adhabu yake itakuwa ni shilingi 50,000/=, vilevile atapunguziwa alama 10.

Hii ni kwamba dereva akishathibitishwa atapewa alama 100 ambazo zitakuwa zinapungua akibainika na

makosa mbalimbali na kwa kila kosa la ya leseni yake ya udereva, uthibitishwa kama inavyooneshisho wa kulipia ada ya kuthibitishwa wa kwenye Jedwali la 5 Sehemu ya A pamoja na taarifa ya daktari inayoya Kanuni za Kuthibitisha Madereva thibitisha afya yake na taarifa hizi zote na Kusajili Wahudumu wa Vyombo ataziwasilisha kwa njia ya mtandao vya Moto Vinavyofanya Kazi Kib-

iashara, (zilizofanyiwa Marekebisho) Dereva atafika kufanya mtihani 2021. Hivyo, anawasihi madereva wa-

kwa kutumia mfumo wa DTS, mfumo jitokeze kwa wingi ili kuthibitishwa na utasahihisha mtihani na kutuma ma-kuepukana na kadhia zinazoweza ku- tokeo ya mtihani kwa dereva kwa njia ya ujumbe mfupi wa maadishi kupitia wafika.

Naye Bi. Esnath Mwakyembe am-

simu yake ya mkononi. Matokeo ya



Baadhi ya madereva waliojitokeza kufanya mtihani wa kuthibitishwa kielektroniki inayofanyika katika vyumba maalum ya mitihani ofisi za LATRA, Mkoa wa Dar es Salaam

baye ni Kaimu Meneja Uthibitishaji mtihani wa dereva aliyefaulu yatatumwa Madereva na Usajili wa Wahudu- wa pia kwenye mfumo mama kwa ajili mu, anaelezea mfumo wa DTS kuwa ya kuchapisha cheti ambacho kitamni mfumo wa kielektroniki wa kutahini tambulisha kuwa amethibitishwa na madereva, ambapo dereva anatakiwa Mamlaka,” anafafanua Bi. Mwakyem- kujisajili kwa kutumia namba yake be.

ya NIDA kwenye mfumo mama wa RRIMS kupidia anuani ya <https://rrims.kwamba.tz/>. “Tafiti mbalimbali zinaone-latratr.go.tz/login na kuweka nafasi ya sha kuwa chanzo kikubwa cha ajali ni kufanya mtihani (booking) na kisha makosa ya kibinadamu na hivyo Ser-kuchagua tarehe na muda atakaopenda ikali kupitia LATRA inafanya kila jitihada ili kupunguza ajali nchini hasa

Vilevile anaongeza kuwa, ili dereva kwa vyombo vya abiria vinavyodhibi-asajiliwe, anatakiwa kuwasilisha che-tiwa na mamlaka, kwani mamlaka ina- ti cha chuo alichosomea udereva wa wajibu wa kuimarisha usalama katika kuendesha magari ya biashara kutoka sekta zinazodhibitiwa. Hivyo, ina- kwenye chuo kinachotambulika, naka- tumia teknolojia za mifumo kama vile

**Inaen-delea UK 7**



## UTHIBITISHAJI WA MADEREVA NI TIJA YA KUBORESHA.....

### Inatoka Uk 7

Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari -VTS na DTS ili kutimiza wajibu huo.”

Vilevile, kuhusu mfumo unavyofanya kazi, Bi Mwakyembe anawakumbusha madereva wote kuwa, mfumo hauruhusu udanganyifu wa aina yoyote kwa kuwa unasahihisha mtihani na kutoa matokea. Hivyo anawasihi madereva wote kufanya maandalizi ya kutosha kwa kupitia mambo yote waliyosoma ili wafanye vizuri katika mitihani, kwani mitihani hiyo imetungwa kwa kufuata mitaala ya vyuo vilivyopata ithibati ya kutoa mafunzo ya udereva.

Naye Bw. Jerive Malaki, Ofisa Leseni na Udhibiti LATRA anasema kwamba udereva ni fani ya kitaaluma kama zilivyo taaluma nyingine amba zo vigezo na masharti ya kitaaluma huzingatiwa. Hivyo madereva walipitia mafunzo na kufuzu wanahimizwa kujitokeza ili wathibitishwe katika fani yao ya udereva. Kazi ya kuthibitisha madereva itasaidia kuwachuja na kubaki na madereva wenye uwezo na sifa stahiki za kuendesa magari ya kibiashara ili kuongeza tija na ufansi katika sekta ya usafiri kwa njia ya barabara.

Bw. Malaki anaongeza kuwa, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu ya barabara ambapo mikoa karibu yote nchini imeunganishwa kwa barabara za lami, hivyo ni muhimu kuwa na madereva wanaokidhi mabadiliko ya teknolojia na maendeleo makubwa tuliyonayo.

Aidha, anasema kumekuwa na



## DEREVA WA CHOMBO CHA USAFIRI KIBIASHARA

### FANYA MTIHANI UTHIBITISHWE

- Utambulike rasmi
- Ufungue fursa kimataifa
- Uimarische usalama barabarani

JISAJILI KUPITIA  
[rrims.latra.go.tz](http://rrims.latra.go.tz)

malalamiko mengi kuhusu uwepo wa Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afmadereva wasiozingatia maadili ya rika (SADC).

fani ya udereva kwa kufanya kazi kwa mazoea hivyo kuchafua kazi na taalu- hizo yatakuwa na mfumo mmoja wa ma ya udereva. Mfumo wa kutahini mafunzo, utahini na uthibitishaji madereva umekuja kutatua changamo- dereva ambapo watakaokidhi vigezo to ya makosa ya kibinadamu yanayo- watapewa vibali vinavyowaruhusu sababishwa na madereva wachache kuendesa gari katika nchi hizo endawasiozingatia taaluma ya udereva.

“Mataifa wanachama wa jumuiya hizou na mfumo mmoja wa ma ya udereva. Mfumo wa kutahini mafunzo, utahini na uthibitishaji madereva umekuja kutatua changamo- dereva ambapo watakaokidhi vigezo to ya makosa ya kibinadamu yanayo- watapewa vibali vinavyowaruhusu sababishwa na madereva wachache kuendesa gari katika nchi hizo endawasiozingatia taaluma ya udereva.

“Kwa kutumia Kanuni za LATRA husika au kuajiriwa huko. Madereva za uthibitishaji madereva, thamani waliothibitishwa na LATRA watanu- ya madereva itapanda na kuwafanya faika na mfumo huu kwani vigezo vyao wafanye kazi kwa kujiamini, kwani vimezingatia protokoli za kimataifa,” hakuna dereva atakayeendesha gari alisema. la kibiashara kama hajathibitishwa na mamlaka, hivyo upatikanaji wa dereva kuwa, dereva anayethibitishwa na utapaswa kuzingatia utaratibu maalu- mamlaka atapatiwa kifaa maalumu mu hali itakayoondoa vitisho na ku- atakachotakiwa kukigusisha kwenye fukuzana bila utaratibu kwa madereva Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa wanaozingatia maadili ya taaluma yao, Magari (VTS) kila anapoanza saf- Hivyo, madereva wasio na sifa ha- ri ambacho kitamsaidia kumkumbu- watakuwa na nafasi tena,” anasisitiza sha muda anaotakiwa kupumzika au Bw. Malaki.

Vilevile CPA Suluo anaongeza mamlaka, hivyo upatikanaji wa dereva kuwa, dereva anayethibitishwa na utapaswa kuzingatia utaratibu maalu- mamlaka atapatiwa kifaa maalumu mu hali itakayoondoa vitisho na ku- atakachotakiwa kukigusisha kwenye fukuzana bila utaratibu kwa madereva Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa wanaozingatia maadili ya taaluma yao, Magari (VTS) kila anapoanza saf- Hivyo, madereva wasio na sifa ha- ri ambacho kitamsaidia kumkumbu- watakuwa na nafasi tena,” anasisitiza sha muda anaotakiwa kupumzika au Bw. Malaki.

Akizungumzia faida za mfumo shaendesa kwa umbali ambao kitaala- huo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, CPA mu anakuwa amechoka.

Habibu Suluo anaeleza kwamba, pindi dereva anayeendesha chombo cha us- uthibitishaji wa madereva utasaid- afiri kibiashara anaposajiliwa na kuth- ia kuipandisha hadhi taaluma ya ud- ibitishwa na mamlaka atatambulika ereva ambapo ni vigumu kwa dereva kwenye Jumuiya za Afrika Mashari- mwenye uzoefu wa miaka 10 bila ajali ki, Soko la Pamoja la Nchi za Kusini kulingana na yule wa miaka mitano mwa Afrika (COMES) na Jumuiya ya mwenye ajali kila mwaka mathalani.



## UTHIBITISHAJI WA MADEREVA NI TIJA YA KUBORESHA.....

**Inatoka Uk 9**

Hivyo kazi hii inatarajiwa kuwachuja madereva kulingana na uzoefu na weledi kazini, hatua ambayo itasidia kupandisha hadhi ya kazi ya udereva, tofauti na ilivyo sasa ambapo kumekuwa na malalamiko ya wamiliki kuajiri madereva wasio na sifa stahiki na hivyo kuchangia ajali za barabarani na kuishusha thamani ya udereva.

Naye Bw. Remmy Mbonda, dereva wa lori anasema kuwa kuna umuhimu wa kusajiliwa, kutahiniwa na kuthibitishwa na LATRA. Anasema, "Mtihani huu unamsaidia dereva kujitambua, fani ya udereva kutambulika rasmi na Serikali, hivyo mimi kama dereva nitakuwa najiamini kwani natambulika rasmi, hivyo naweza kufanya kazi nchi yoyote. Niwasihii tuu madereva wengine wajitokeze kwa wingi na kuthibitishwa na LATRA."

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA Suluo, mpaka sasa zaidi ya madereva 200 wamefanya mtihani na kati yao madereva waliokidhi vigezo vya kuthibitishwa na mamlaka watapewa vyeti vitakavyoambatana na masharti ambayo dereva hatatakiwa kuyavunja.

Aidha, kwa wale ambao havakukidhi vigezo vya kuthibitishwa, wanapewa nafasi ya kuijandaa vizuri na kurudia mtihani ili kuhakikisha kila dereva anapata haki yake kisheria ya kuthibitishwa na hivyo Serikali kupata matokeo chanya kwa kupunguza ajali zinazoweza kuepukika.

## TUTUMIE TIKETI MTANDAO KWA MANUFAA YETU SOTE



Tiketi Mtando ni tiketi zinazotolewa kwa njia ya kielekroni ambapo pindi abiria anapokata tiketi hiyo anapata ujumbe mfupi wa maandishi kwa njia ya simu ya mkononi au anapewa risiti kutoka kwenye mashine maalum ikionyesha majina yake na taarifa zake na safari husika. Tiketi hizi ni tofauti na zile tiketi ziizokuwa zikitumika awali ambazo zilikuwa zin-aandikwa kwa mkono na kusababisha changamoto kubwa kwa abiria.

Amina Bakari, mkazi wa Dar es Salaam anelezea namna alivyopata shida na mfumo wa zamani wa ukatishaji tiketi, na kuishukuru Serikali kwa hatua ya uanzishaji wa mfumo wa tiketi mtando.

"Naishukuru Serikali kwa kutuletea tiketi hizi za mtando kwa sababu nilikuwa napata bughudha sana pindi nilipotaka kusafiri. Ilikuwa nikienda kwenye kituo cha mabasi nagombaniwa kama bidhaa na wakati mwagine kiti kimoja tunakatiwa tiketi zaidi ya mtu mmoja. Basi ilikuwa ni vurugu sana ila kwa mfumo huu mpya wa Tiketi Mtando kwa kweli mambo yamekuwa rahiisi sana. Mimi kwa kutumia simu yangu

ya mkononi tu nakata na kulipia tikitiki kwa basi ninalolitaka na nachagua kiti ninachokitaka bila shaka yoyote, Halikadhalika, Tiketi Mtando zinatuondolea uwezekano wa kupandishiwa nauli kiholela," alisema Amina.

Maandalizi ya Mfumo wa Tiketi Mtando ni mchakato ambao umewahusisha wadau mbalimbali. Kwa mfanano, baada matumizi ya mfumo kuanza wadau waliibua changamoto mbalimbali zilizoifanya serikali kuunda Kamati Maalumu kwa ajili ya kushughulikia changamoto hizo.

Kamati hiyo ilikuwa na wajumbe 11 ambapo wajumbe watano (05) wa upande wa Serikali walitoka LATRA, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu Kimtando (NIDC) na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na wengine sita (06) walitoka sekta bin afsi hususan Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA). Kamati hiyo ilitoa mwelekeo mpya wa mfumo kwa kuondoa changamoto zilizojitokeza hapo awali.

Akizungumzia historia ya Mfumo huo, Meneja wa Mradi wa Tiketi **Inaendelea UK 10**



# TUTUMIE TIKETI MTANDAO KWA MANUFAA....

## Inatoka Uk 9

Mtandao LATRA, CPA Tadei Mwita anasema kuwa kipindi cha nyuma abiria walikuwa wakigombaniwa kama bidhaa kwenye vituo vya mabasi na wakati mwagine walikuwa wakipele-kwa kwenye mabasi ambayo hawaku-wa wameyachagua kusafiri nayo hali ambayo lilikuwa linaleta usumbufu mkubwa kwa abiria na wamiliki wa mabasi.

Wamiliki walikuwa wakiathirika kwa sababu ya kushindwa kupata fedha kamili ya mauzo ya tiketi kwenye mabasi yao. Kiasi kikubwa cha fedha wa wamiliki kilipotelea mikononi mwa walangazi na madalalali wa tiketi.

Vilevile CPA Mwita anaongeza kuwa changamoto hizo ndizo ziliifanya mamlaka na wadau wake kupata wazo la kutengeneza utaratibu muhususi ambao utasaidia kuondoa changamoto hizo kwa kumwezesha abiria ajikatie tiketi popote alipo na wakati wowote anaoutaka kupitia simu yake ya mikononi ambayo ni simu janja.

Aidha, CPA Mwita anafafanua zaidi kuwa, baada ya mamlaka kuanzishwa mwaka 2019, ilipofika mwaka 2020, zilitungwa kanuni mbalimbali ikiwemo Kanuni za Leseni za Usafirishaji za Magari ya Abiria ambapo Kanuni ya 4(2)(c) inasema kuwa mamlaka isitoe leseni kwa msafirishaji ambaye hajaunganishwa kwenye mfumo wa tiketi za kielektroniki ulioidhinishwa na mamlaka.

Kanuni hizo zinaenda mbali zaidi ambapo Kanuni ya (22)(j) inawataka wasafirishaji wote kuhakikisha wanatumia mfumo wa kielektroniki kutoa tiketi zao na Kanuni ya 24 inamtaka msafirishaji kutoa tiketi za kielektron-

iki kwa abiria wote anaowasafirisha. janja au endapo abiria atapata chan-Kwa hiyo mfumo huu umetengenez-gamoto za kutumia mfumo ni kwenda wa na unatumika kwa mujibu wa ka-kwenye kituo cha mabasi na kukata nuni kwa hiyo msafirishaji anayekiuka tiketi ya mtandao kwa wakala wa basi basi afahamu kuwa anakiuka kanuni husika ambaye atampatia abiria tiketi zilizowekwa na mamlaka ambayo ni kupitia mashine maalumu. makosa.

Vilevile CPA Mwita anaeleza kuwa

Akielezea namna mbalimbali za wapo baadhi ya wasafirishaji ambao kukata Tiketi Mtandao, CPA Mwi-wameenda mbali zaidi kwa kufanikisha ta anasema kwamba abiria anatakiwa ukataji wa tiketi kwa njia ya mitandau kuingia kwenye mtandao na kupakua ao ya kijamii kama WhatsApp, amba-mfumo tumizi (application) wa tike-po abiria unatuma ujumbe mfupi kwa ti mtandao na kuhifadhi kwenye simu njia ya WhatsApp na kisha unasema



*CPA Tadei Mwita akizungumzia tiketi mtandao kwenye mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Makao Makuu ya LATRA, Dar es Salaam*

janja yake na akitaka kuitumia, ataifun-unataka kusafiri kwenye njia gani, kiguwa, atachagua lugha anayoitaka kama sha utatajiwa nauli na kupatiwa namba ni Kiswahili au Kiingereza kisha ata-ya kumbukumbu kwa ajili ya malipo chagua anakotaka kwenda na kwenye na tiketi yako utaiona papohapo. Kwa mfumo kuna kalenda ambayo ataitumia hiyo kwa sasa sasa mfumo umekuwa ni rachagua tarehe anayotaka kusafiri. hisi sana kutumia.

Pia abiria atachagua daraja la basi kama vile daraja la juu, kati au mfumo wa tiketi mtandao hadi kufikia la kawaida na kisha atachagua kiti tarehe 17 Agosti, 2022, Mkurugenzi anachotaka kukaa na atajaza taarifa Mkuu wa LATRA, CPA Habibu Suluo zake. Kisha mfumo utamuelekeza na amesema hadi sasa jumla ya mabasi atapata namba ya malipo anayoweza 2,033 yanayomilikiwa na kampuni 308 kulipia kuitia mitandao ya simu na ki-za usafirishaji abiria yameshaunganish-sha atapata tiketi yake kuitia ujumbe wa kwenye mfumo wa Tiketi Mtandao mfupi wa maandishi. kuitia watoa huduma (vendors).

Aidha, njia nyingine ya kutumia mfumo, kwa wale ambao hawana simu ya mabasi 7,649 yamesajiliwa kwenye “Hadi kufikia Agosti 17, 2022, Jumla Inaendelea UK 11



# TUTUMIE TIKETI MTANDAO KWA MANUFAA....

**Inatoka Uk 10**

Mfumo wa Ufuatiliaji Mwenendo wa Magari- VTS ambapo mabasi 3,916 yameonekana yapo barabarani (active). Mafanikio haya ni sawa na asilimia 52 ukilinganisha na asilimia 37 ilivyokuwa Julai 31, 2022,” anasema CPA Suluo.

Anaongeza kuwa, LATRA imetekeleza maboresho ya mfumo wa Tiketi Mtandao kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu Kimtandao (NIDC), Watoa Huduma za Tiketi za Kielektroniki na wadau wengine wa serikalini na sekta binafsi.

Aidha, mamlaka kwa kushirikiana na wadau hao, walifanya kazi ya kuainisha changamoto zilizojitokeza katika mfumo, na baada ya kujiridhisha, wadau wote walikubaliana kutoa muda wa mfumo wa Tiketi Mtandao kufanya kazi kwa majaribio kabla ya kuanza rasmi.

“Tunawapongeza wasafirishaji na wadau wote walioshiriki kutimiza takwa la kisheria la mabasi husika kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao. Nitumie nafasi hii pia kuwakumbusha wadau kuwa tunaenda kuuchukua hatua stahiki, ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu ya fainina/au kusitisha huduma ya mabasi yote ambayo yatashindwa kutimiza takwa hili la kisheria ifikapo tarehe 1 Septemba, 2022,” anaeleza CPA Suluo.

Aliendelea kueleza kuwa matumizi ya tiketi za kielektroni yamelenga kuwanufaisha wasafirishaji, abiria na Serikali. “Kupitia mfumo huu wasafirishaji wanaweza kudhibiti mauzo ya abiria, namba ya basi, tarehe na muda



*Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA HAbibu Suluo (katikati) akikagua tiketi ya kielekroni wakati wa ukaguzi wa kushtukiza katika Kituo cha Mabasi Magufuli*

tiketi kwa kuwa mfumo unawaweze- wa safari, kituo cha kuanzia na kumalsha kuona mauzo yote yanayofanyika izia safari, nauli iliyolipwa, anwani na kupitia simu za mkononi. Ni matarajio namba za simu za msafirishaji na namyetu kuwa matumizi ya mfumo ya- ba ya tiketi husika.”

Aidha, anaongeza kuwa taarifa sa-

huduma zao kwa kuongeza uwekezaji hihi za abiria katika mfumo wa Tiketi

kwenye sekta,” anasema. Mtandao ni muhimu kwa kuwa zinawe-

Aidha, CPA Suluo pia anawasihi ka kumbukumbu sahihi za safari husika wamiliki wa mabasi kuingiza mabasi na iwapo kukitokea tatizo itakuwa raya kwenye mfumo ili kuwarahisishia hisi kuthibitisha taarifa za safari hiyo, wananchi pindi wanapotaka kusafiri kwa kukata tiketi hizo kwa mtan-

dao na anasema kuwa kwa mmiliki tofauti, kwa mfano ikitokea ajali na atakayekaidi atakuwa anatenda kosa.

Alifafanua zaidi kuwa, wamiliki abiria huyu kupata stahiki zake ikiwa

hao wa mabasi wakiyaingiza magari ni pamoja na fidia ya bima,” anasema. Katika kikao cha tathmini ya mfuhamu usalama wa magari barabarani mo wa tiketi mtandao kilichofanyika ikiwa ni pamoja na kuona kama yanak-hivi karibuni katika ofisi za Makao wenda kinyume cha mwendo unaotaki- Makuu ya LATRA Dar es Salaam, wa pindi yanapokuwa katika safari zao Naibu Kamishina wa Kodi TRA, Bw. kila siku jambo ambalo litaongeza us-alama wa safari zao pamoja na abiria awali kulikuwa na hoja zilizowasilishwa na wasafirishaji kupitia TABOA iki-

Vilevile CPA Suluo anasisitiza kuhusu taarifa za msingi zinazotakiwa kwa kiwango mfuto (flat rate) ambapo

kuwekwa kwenye tiketi na anasema Serikali imesikia na imeridhia na kwa “Mamlaka inawakumbusha wamiliki sasa wasafirishaji wa mabasi watatozwa mabasi kuhakikisha kuwa tiketi ina wa kwa kiwango mfuto kulingana na taarifa zote muhimu ikiwemo jina la uwezo wa gari kubeba abiria.

Naye Bw. Abdallah Kiongozi  
**Inaendelea UK 12**

788899920000

ali kuthibitisha  
io, hakiki taarifa na  
elea'.

apepe na taarifa  
kwenye fomu ya usai

ni;  
mba ya cheti  
ha usajili wa  
swali kuthibi  
isho wa kam

*Mkurugenzi Udhiliti Usafiri wa Barabara - LATRA Bw. Johansen Kahatano akisisitiza matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao*

## TUTUMIE TIKETI MTANDAO KWA MANUFAA....

### Inatoka Uk 11

Mwenyekiti TABOA anaeleza kuwa mfumo wa Tiketi Mtandao ni bora na mzuri ambao utawasaidia wamiliki wa mabasi, watumishi, mamlaka za Serikali pamoja na abiria na ametoa wito kwa wasafirishaji na wamiliki kuunga mkoно Serikali kwenye jambo hilo muhimu kwa maendeleo ya nchi. Wamiliki watanufaika sana kwa kuwa kupitia mfumo huu, fedha zitakazokusanya zinaenda moja kwa moja kwenye akaunti zao.

Akzungumzia faida za mfumo huo, Mkurugenzi wa Udhiliti Usafiri wa Barabara, Bw. Johansen Kahatano anasema mfumo huo una faida lukuki kwa abiria, mmiliki wa basi husika na Serikali kwa jumla.

Kwa upande wa abiria, watanufaika na matumizi ya mfumo kwa kwezeshewa kukata tiketi kutokea mahali popote na kuepukana na adha za wapiga debe ukizingatia kuwa kupitia mfu-

mo huu abiria anaweza pia kukata tiketi yake kwa wakala wa benki au wa simu za mitando yote hapa nchini. Pia mfumo utawaepusha abiria na adha ya upandishaji nauli kiholela kwa kuwa nauli zimebekwa ndani ya mfumo.

Kwa upande wa Serikali, itanufaika kwa taarifa zinazozalishwa na mfumo kwa kupata taarifa mbalimbali zitakazosaidia kufanya maamuzi muhimu yakiwemo ya kuboresha huduma, miundombinu na kukokotoa kodi ya mapato.

Kwa upande wa mmiliki, kwa kutumia mfumo huu, mmiliki atakuwa anaona na kupata malipo yake moja kwa moja na hivyo kunufaika kimapato jambo ambalo kwa mfumo wa zamani mmiliki hakuwa anapata taarifa hizi muhimu za mapato yake.

Vilevile Bw. Kahatano anawasihi wananchi ambao ndio abiria wa mabasi hayo kuwa na utaratibu wa kuomba tiketi mtandao pale wanapotaka kusafiri ili kuepuka usumbufu na msongamano kwenye ofisi za ukatishaji tiketi.

Pia anasisitiza kuwa, abiria akishapata namba ya malipo anatakiwa kulipia ndani ya dakika 15 baada ya hapo kama



abiria hajalipia kitu kitakuwa wazi kwa mtaa mwingine mwenye uhitaji wa kusafiri kutumia basi husika.

Halikadhalika Bw. Kahatano anaongeza kuwa, abiria anapotumia mabasi yanayotumia mfumo wa Tiketi Mtandao ataepuka usumbufu pale ambapo mabasi yasyo taka tiketi hizo zitakapozuiliwa kutoa huduma,

"Jambo hili ni la kwetu sote na tunawasihi abiria kuwa mstari wa mbele kwenye kudai tiketi za kielektroniki kwenye mabasi. Abiria ukipewa tiketi ya makaratasi kataa na dai ile ya kielekroni, kumbuka tiketi yako ndio mkataba wako na mwenye gari ulilopanda."

Hakika mfumo wa tiketi mtandao ni mwarobaini kwa kadhia walizokuwa wakipata abiria hapo awali na pia ni jambo la furaha kwa mmiliki kwa kuwa inawaepusha na hasara ambazo walikuwa wakizipata kabla ya mfumo huu na pia unaleta tija kwa Serikali hasa kwenye kupata takwimu na kupanga mipango ya usafiri hivyo basi muhimu kwa wananchi wote kutumia mfumo huu kwa maendeleo ya taifa kwa jumla. Ikumbukwe kuwa, mara baada ya kukata Tiketi Mtandao, abiria ataipata tiketi hiyo kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi unaotumwa kwenye simu yake au atapatiwa karatasi maalumu iliyochapishwa kwenye mashine ya kutolea tiketi.



- ABIRIA tumia Tiketi Mtandao, Rahisisha Maisha
- Ingia Playstore/Appstore katika simu janja
- Pakua Tiketi Mtandao kisha fuata maelekozo
- Nunua tiketi bila kwenda kituo cha mabasi
- Usikubali kununua tiketi iliyoadikwa kwa mkoно
- Epuka kero za wapigadebe
- Pata uhakika wa safari yako
- Epuka kugonganishwa nafasi ndani ya basi
- Okoa gharama za kwenda kwenye ofisi ya mtoa huduma kununua tiketi

LATRA kwa Usafiri Bora na Salama

LATRA MAMLUKA YAMAPATO TANZANIA

Institusisheni ya ISO 9001:2015



www.latra.go.tz 0800110019 info@latra.go.tz



# LATRA KUONGEZA USHIRIKIANO KIUDHIBITI KATI YA TANZANIA NA AFRIKA KUSINI

Kutoka Uk 5

kwa mapokezi na kuridhia kikao kazi  
hicho ambapo amesema kitaongeza  
ufanisi katika taasisi yao pindi wa-  
takaporudi.

“Nawashukuru kwa kukubali ku-kaa nasi na kushiriki katika kikao kazi hiki ambapo mbali na kuwa ni moja ya ishara ya ushirikiano baina ya nchi zetu (Tanzania na Afrika Kusini), pia kitatusaidia kujua mbinu na mikakati itakayowezesha kuongeza ufanisi katika shughuli za udhibiti nchini kwetu, hivyo tunategemea kujifunza mengi kutoka kwenu,” amesema Mafuraha.

Katika kikao kazi hicho, wajumbe hao wameelezwa shughuli za mammalaka pamoja na namna LATRA inavyotekeleza Sheria na Kanuni za Udhhibit Usafiri Ardhini nchini na kimehudhuriwa na wajumbe kutoka C-BRTA Afrika Kusini pamoja na Menejimenti ya LATRA.

# WASAFIRISHAJI WAITIKIA TIKETI MTANDAO



**M**amlaka ya Udhibiti Usafiri 2022," ameeleza CPA Suluo. Ardhini (LATRA) kupitia Akizungumzia manufaa ya mfum Mkurugenzi Mkuu, CPA Habibu Su- mo huu ameongeza kuwa matumizi luo imebainisha mwitikio chanya kwa ya tiketi za kieletroniki yamelenga wamiliki wa mabasi ya masafa marefu kuwanufaisha wasafirishaji, abiria na katika kuijunga na kutoa tiketi kielek- Serikali, na kupitia mfumo huo wasa troniki kupitia mfumo wa tiketi mtan firishaji wanawenza kudhibiti mauzo ya dao tangu mfumo huu uanzesha kutumika tiketi kwa kuwa mfumo unawawez rasmi Julai 1, 2022. sha kuona mauzo yote yanayofanyika

Kwa nyakati tofauti, CPA Habibu kuitia simu za mkononi.

Suluo amekuwa akitoa tathmini ya “Ni matarajio yetu kuwa matumizi mwenendo wa tiketi mtandao, akizuya mfumo yatawawezesha wasafirungumza kwenye mkutano na waan- ishaji kuimarisha huduma zao kwa dishi wa habari uliofanyika ofisi za kuongeza uwekezaji kwenye sekta. mamlaka zilizopo Mkoa wa Dar es Abiria watanufaika na matumizi ya Salaam Agosti 18, 2022, CPA Suluo mfumo kwa kuwezeshera kukata tiketi alisema jumla ya mabasi 2,033 yan- kutokea mahali popote na kuepukana ayomilikiwa na kampuni 308 za us- na adha za wapiga debe,” amefafanua. afirishaji abiria yameshaunganishwa Ili kuboresha mfumo wa tike- kwenye mfumo wa Tiketi Mtandao ti mtandao, mfumo ulikuwa katika kupitia watoa huduma (vendors). kipindi cha majaribio kuanzia Aprili

"Hadi kufikia tarehe 17, Agosti, Mosi 2022 hadi Juni 30, 2022. Tarehe 2022, Jumla ya mabasi 7,649 yamesa- mosi Julai, Mamlaka ilitoa muda wa jiliwa kwenye Mfumo wa Ufutiliaji nyongeza wa miezi miwili hadi tare- Mwenendo wa Magari- VTS amba- he 31 Agosti, 2022, ulioambatana na po mabasi 3,916 yameonekana yapo kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa barabarani (active). Mafanikio haya wasafirishaji waliokuwa na chan- ni sawa na asilimia 52 ukilinganisha gamoto tofauti tofauti ili kuhakikisha na asilimia 37 ilivyokuwa Julai 31, mabasi yote yaunganishwe kwenye

Inaendelea UK 17

- ABIRIA tumia Tiketi Mtandao, Rahisisha Maisha
  - Ingia Playstore/Appstore katika simu janja
  - Pakauna Tiketi Mtandao kisha fuata maelekozo
  - Nunua tiketi bila kwenda kituo cha mabasi
  - Usikubali kununua tiketi iliyoandikwa kwa mkono
  - Epuka keru za wapigadebe
  - Pata uhakika wa safari yako
  - Epuka kugonganishwa nafasi ndani ya basi
  - Okoa ghamara za kwenda kwenye ofisi ya mtoau humuduma kununua tiketi



# KATIBU MKUU - UCHUKUZI AMKABIDHI OFISI MKURUGENZI MKUU MPYA LATRA



*Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Gabriel Migire wakati wa kukabidhi ofisi kwa Mkurugenzi Mkuu mpya wa LATRA CPA Habibu Suluo*

**K**utokana na uteuzi uliofanywa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua CPA Habibu J.S Suluo kuwa Mkurugenzi Mkuu wa LATRA Julai 9,2022, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Gabriel Migire amemkabidhi ofisi Mkurugenzi Mkuu mpya wa LATRA, CPA Habibu J. Suluo tarehe 11 Julai, 2022 baada ya kufanya kikao na Menejimenti ya LATRA katika Ukumbi wa Makao Makuu ya LATRA jijini Dar es Salaam.

Katika kikao hicho, Bw. Migire amewasihi wafanyakazi wa LATRA kuchapa kazi kwa juhudini na maarifa ili kufikia matarajio ya wizara na Serikali kwa ujumla katika kutoa

huduma kwa wananchi hususan katika kuboresha ufanisi wa mfumo wa Tiketi Mtandao na Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS).

“LATRA ina nafasi kubwa katika sekta ya usafiri ardhini, na ikifanya kazi vizuri itachangia sana ukuaji wa uchumi, hivyo Serikali na wizara ina matarajio makubwa kwa Mamlaka hii.” ameeleza.

Aidha, Katibu Mkuu amesisitiza LATRA kufanya kazi kwa ukaribu na wadau mbalimbali ili kushirikiana kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya usafiri ardhini.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, CPA Habibu Suluo amemshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kumteua na kuwa amepokea uteuzi huo kwa heshima na kumshukuru Mkurugenzi Mkuu aliyemaliza muda wake Bw. Gilliard Ngewe kwa mafanikio yaliyofikiwa na mamlaka wakati wa uongozi wake.

Aidha, CPA Suluo ameahidi kufanya kazi kwa ukaribu na wadau mbalimbali ikiwemo wafanyakazi wa LATRA ambao kwa kiasi kikubwa anawafahamu kwa muda mrefu alio-wahi kufanya nao kazi.

Aliongeza kuwa anazifanahamu changamoto nyingi za usafiri ardhini, hivyo atashirikiana na timu ya wafanyakazi wa LATRA kuzitatua changamoto hizo na kuendeleza mazuri yaliyoanzishwa na kuboresha zaidi.



# LATRA YAENDESHA MKUTANO WA WADAU KUTATHMINI MFUMO WA TIKETI MTANDAO

Baada ya mfumo wa Tiketi Mtandao kuanza kufanya kazi rasmi Julai 1, 2022, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imefanya mkutano na wadau wa usafirishaji Julai 21, 2022 ili kutathmini utekelezaji wa mfumo huo na kujadili changamoto zinazojitokeza ili kuzifanyia kazi.

Mkutano huo umejumuisha wadau mbalimbali wakiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu Kimtandao (NIDC) pamoja na watoa huduma za mifumo ya utoaji tiketi kielektroniki.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA Habibu J. Suluo amesema mkutano huo umeazimia kuwa tiketi zote za mabasi ya masafa marefu zitatolewa kwa mfumo wa Tiketi Mtandao na kuwa mamlaka inaendelea kufanya kaguzi na kutoa elimu kabla ya kuanza kutoa adhabu.

“Tunaendelea kutoa elimu kuhakikisha wananchi wanaelewa, na wale ambao bado hawajaingia kwenye mfumo wanaingia, kwa kuanzia tunakutana kila mwezi ili kuendelea kutatta changamoto na kuhakikisha mababiliko ya mfumo huu yanazoeleka,” alisema.

Kwa upande wake, Naibu Kamishna wa Kodi za Ndani wa TRA, Bw.



*Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA Habibu J. Suluo (katikati), Kamishna wa Kodi za Ndani wa TRA, Swalehe Byarugaba (kushoto) na Mwenyekiti wa TABOA, Abdallah Kiongozi katika mkutano na wadau wa Tiketi Mtandao*

Swalehe Byarugaba alisema “Lengo la mkutano huu ni kuhakikisha msafirishaji Barabara LATRA, Johansen Kahatano anakawa na nyaraka moja ambayo ita- amesema kwa mfumo wa Tiketi Mtan- simama kama risiti na wakati huohuo dao kwa sasa umeboreshwa baada ya kama tiketi ya abiria, nashukuru uon- changamoto mbalimbali zilizokuwepo gozi wa TABOA na wadau wengine, kupatiwa ufumbuzi kwa kushirikisha tumekubaliana tiketi zote zitolewe Serikali na wamiliki wa mabasi. kwa njia ya mtandao.”

Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa mfumo huu ni mzuri kwa kuwa una- zote Tanzania Bara katika kazi ya ku- kao hicho ni mwendelezo wa kubore- toa elimu na kupokea maoni iliyofan- sha mfumo wa tiketi mtandao na kuwa yika kwa miezi mitatu ya Aprili, Mei mfumo huu ni mzuri kwa kuwa una- na Juni 2022. wasaidia wamiliki, mamlaka za Seri- kali na Abiria, huku akiwaasa wana- nchi na wasafirishaji kuunga mkono juhudzi za Serikali.



# LATRA, POLISI KUKOMESHA UKIUKWAJI WA MASHARTI YA LESENI

**N**aibu Waziri wa Mambo ya Simiyu kwa kuchukua hatua za kudhibiti ya leseni. Kwa upande wa mabasi yan- Ndani ya Nchi ambaye pia ni matumizi ya magari yaliyosajiliwa kama ayoenda mikoani tumeshachukua hatua Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Us- tekxi yanayokiuka sheria na kubeba na kwa sasa hivi hatutoi leseni bila basi alama Barabarani, Mhe. Jumanne Sagini abiria wa masafa marefu.

(MB) ameelekeza Jeshi la Polisi Kiko- si cha Usalama Barabarani pamoja na fanya tathmini na kujiridhisha kuwa VTS. Kanuni za Leseni za usafirishaji Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini magari hayo yalikuwa yakikiuka she- (LATRA) kushirikiana kuptitia idadi ya ria za usalama barabarani na masharti zinataka abiria kupatiwa tiketi ya kielek- magari madogo yaliyopewa leseni za ya leseni kwa kiasi kikubwa ikiwemo troniki, ambapo kwa sasa tunaendelea usafirishaji na kutathmini ukiukwaji wa kubeba abiria wengi kuliko uwezo wa na kampeni kuhakikisha kuwa mabasi masharti ya leseni nchi nzima na ku- chukulia hatua za kisheria madereva na wamiliki wanaokiuka mashari ya leseni zao.

Mhe. Sagini amesema hayo Julai 22, 2022 kwenye mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika Ukumbi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi jiji- ni Dar es Salaam.

Katika mkutano huo, Mhe Sagini amesema kuwa Serikali inataku kuona vyombo vinavyotembea barabarani vinazingatia sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani. Ametaka kuen- delea kutoa elimu kwa abiria na kushau- ri kutumia usafiri wa mabasi au vyombo vingine vya moto vilivyoruhusiwa kwa mujibu wa sheria, "kwenye hili nawaom- ba abiria ambao ni wananchi wenzetu wasiwe sehemu ya kukiuka sheria".

Aidha, Mhe. Sagini amewasihi wasa- firishaji wenyе magari yanayokidhi vigezo vya kusafirisha abiria kuomba leseni kwenye maeneo yenye uhitaji kama vile mikoa ya Simiyu, Kagera, Ki- goma, na kadhalika ili kupunguza adha ya usafiri katika maeneo hayo.

Amesititiza kuwa LATRA na Jeshi la Polisi kuptitia Kikosi cha Usalama Barabarani kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala muhimu ya us- alama kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Pia Mhe. Sagini ameipongeza Ka- mati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoo wa

Uamuzi huo ni baada ya kamati ku- wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari – fanya tathmini na kujiridhisha kuwa VTS. Kanuni za Leseni za usafirishaji Mamlaka ya abiria za mwaka 2020 (LATRA) kushirikiana kupatiwa tiketi ya kielek- magari madogo yaliyopewa leseni za ya leseni kwa kiasi kikubwa ikiwemo troniki, ambapo kwa sasa tunaendelea usafirishaji na kutathmini ukiukwaji wa kubeba abiria wengi kuliko uwezo wa na kampeni kuhakikisha kuwa mabasi



*Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Jumanne Sagini (MB) (kulia) na Mkuru- genzi Mkuu LATRA CPA Habibu Suluo katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika ukumbi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Dar es Salaam*

gari, kuendesha kwa mwendokasi pamo- yanatoa tiketi hizo," amesema CPA Su- ja na ubovu wa magari.

Naye Mkurugenzi Mkuu LATRA, Aidha, ameeleza kuwa, suala la ajali CPA Habibu Suluo amemshukuru Mhe. ni mtambuka hivyo mamlaka itashirikiana na amesema kuwa LATRA ana na viongozi wa mikoa mbalimbali ili itashirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Kikao hicho kimehudhuriwa na Ka- kutoa elimu kwa watoa huduma za us- manda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, Wilbroad Mutafungwa, ni na kuchukua hatua kwa wanaokiuka maofisa wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, wakuu wa us- alama barabarani kutoka Kinondoni, Ilala na Temeke pamoja na maofisa wa

"LATRA inafanya kaguzi mbalimba- alama barabarani kutoka Kinondoni, li ikiwemo kukagua viwango vya ubora Ilala na Temeke pamoja na maofisa wa wa huduma zinazotolewa na masharti LATRA.



# WASAFIRISHAJI

## WAITIKIA TIKETI

### MTANDAO

**Kutoka Uk 13**

mfumo huo.

Mamlaka ilitekeleza maboresho ya mfumo wa Tiketi Mtandao kwa kushirikiana na wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu Kimtandao (NIDC), Watoa Huduma za Tiketi za Kielektroniki na wadau wengine wa serikalini na sekta binafsi.

“Tunawapongeza wasafirishaji na wadau wote walioshiriki kutimiza takwa la kisheria la mabasi husika kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao. Nitumie nafasi hii pia kuwakumbusha wadau kuwa tunaenda kuuchukua hatua stahiki, ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu ya faini na/au kusitisha huduma ya mabasi yote ambayo yatashindwa kutimiza takwa hili la kisheria ifikapo tarehe 1 Septemba, 2022,” amesema CPA Suluo.

Vilevile, CPA Suluo amesema kuwa mamlaka inawakumbusha wamiliki wa mabasi kuhakikisha kuwa tiketi ina taarifa zote muhimu ikiwemo jina la abiria, namba ya basi, tarehe na muda wa safari, kituo cha kuanzia na kumalizia safari, nauli iliyolipwa, anwani na namba za simu za msafirishaji na namba ya tiketi husika.

Alifafanua kuwa taarifa sahihi za abiria katika mfumo wa Tiketi Mtandao ni muhimu kwa kuwa zinaweka mabasi yasiyotoa tiketi hizo zitakopokumbukumbu sahihi za safari husika zuiliwa kutoa huduma.



*Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo akielezea mwenendo wa Tiketi Mtandao katika mkuano na waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam*

na iwapo kukitokea tatizo itakuwa rahihi kuthibitisha taarifa za safari hiyo.

“Taarifa za Tiketi Mtandao zin-kwenye kudai tiketi za kielektroni aweza kumsaidia abiria kwa namna kwenye mabasi. Abiria ukipewa tike-tofauti, kwa mfano ikitokea ajali na ti ya makaratasi kataa na dai ile ya abiria kupata madhara, itakuwa rahisi kielekroni, kumbuka tiketi yako ndio abira huyu kupata stahiki zake ikiwa mkataba wako na gari ulilopanda,” ni pamoja na malipo ya bima,” amese-ma.

Naye Mkurugenzi wa Udhibiti Us-afiri wa Barabara, Bw. Johansen Kahanano amesema kuwa LATRA in-awashauri abiria kutumia huduma za mabasi yanayotumia mfumo wa Tiketi Mtandao kwani mfumo huo una faida nyingi kwa abiria, wasafirishaji na Serikali.

Pia abiria atumiapo mabasi yanayotumia mfumo wa Tiketi Mtandao ataepuka usumbufu pale ambapo mabasi yasiyotoa tiketi hizo zitakopokumbukumbu sahihi za safari husika zuiliwa kutoa huduma.

“Jambo hili ni la kwetu sote na tun-

awasihi abiria kuwa mstari wa mbele kwenye kudai tiketi za kielektroni aweza kumsaidia abiria kwa namna kwenye mabasi. Abiria ukipewa tike-tofauti, kwa mfano ikitokea ajali na ti ya makaratasi kataa na dai ile ya abiria kupata madhara, itakuwa rahisi kielekroni, kumbuka tiketi yako ndio abira huyu kupata stahiki zake ikiwa mkataba wako na gari ulilopanda,” ni pamoja na malipo ya bima,” amese-amesitiza Bw. Kahatano.

Naye Meneja Mradi wa Tiketi Mtandao CPA, Tadei Mwita amesitiza





# MHE. LUDIGIJA -TUNZENI MIUNDOMBINU YA RELI

**M**kuu wa Wilaya ya Ilala, Mhe. Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija amewataka wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuwa mabalizi wa dhati katika kuilinda na kuitunza miundombinu ya reli hapa nchini.

Mhe. Ludigija amesema hayo Agosti 19, 2022 akifungua mkutano wa wadau wa kukusanya maoni kuhusu viwango vya nauli za treni za abiria kwa Mkoa wa Dar es Salaam ulioandaliwa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Aidha, Mhe. Ludigija amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa kwa umahiri na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan inafanya juhudzi za kipekee na inatekeleza kazi kubwa ya kuitunza miundombinu ya reli na kuboresha huduma za treni nchini hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anaitunza miundombiu hiyo kwa manufaa mapana ya taifa.

“Niwapongeze sana LATRA kwa kuvashirikisha wadau na hili ndilo jambo ambalo Rais wetu Samia Suluhu Hassan anasisitiza kila mara kwa kuwa huu ndio msingi wa utawala bora na hata nauli zitakazokuja kutangazwa hapo baadae zitakuwa zimezingatia maoni ya wadau wa sekta hii ya reli hapa nchini,” alisema.

Vilevile, Mhe. Ludigija amesema kuwa, kazi ya kukusanya maoni inayofanywa na LATRA ni kwa mujibu wa sheria hivyo, amewasihi wadau hao kuzingatia umuhimu wa kazi hiyo na watimiza wajibu wao kwa kuwa wanawakilisha wadau wengine ambao kutohana na sababu mbalimbali wameshindwa kuhudhuria mkutano huo.

Aidha, Mhe. Ludigija amewapongeza watumishi wa LATRA kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi huku wakitatuwa changamoto zinazojitokeza kwenye sekta wanazosimamia.

“Ni miaka mitatu tu tangu taasisi hii



*Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija akizungumza katika mkutano wa kukusanya maoni kuhusu viwango vya nauli za treni za abiria kwa mkoa wa Dar es Salaam*

iundwe lakini imekuwa ni miongozi mwa taasisi za mfano, binafsi nakupongeza sana Mkurugenzi Mkuu kwa kuwa na timu inayofanya kazi vizuri na inayojituma,” alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu LATRA, CPA Habibu Suluo amesema kwa mujibu wa Kifungu cha 19 cha Sheria ya LATRA, Sura Na. 413 na Kanuni za Tozo (The Land Transport Regulatory Authority (Tariff) Regulations) za Mwaka 2020, LATRA ina jukumu la kupanga na kufanya mapitio ya tozo (nauli) ya huduma zinazodhibitiwa katika usafiri wa ardhini (barabara, reli na waya).

CPA Suluo ameongeza kuwa ili LATRA ipange tozo (nauli), mtoa huduma anayedhibitiwa anapaswa kuwasilisha maombi kwa LATRA. Baada ya kupokea maombi, LATRA humpa mtoa huduma nafasi ya kuwasilisha mapendekezo yake kwa wadau na pia kuwapa fursa wadau kutoa maoni yao juu ya mapendekezo yatakayowasilishwa. Hivyo, LATRA ilipokea maombi ya TRC ili apewe nafasi ya kuwasilisha kwa wadau na leo

ndio wameanza mchakato huo.

“Natoa wito kwa wadau mbalimbali kuitumia vizuri nafasi hii, ili kuwaweza-sha wataalamu wetu wafanye kazi yao kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu,” ameeleza CPA Suluo.

CPA Suluo ameongeza kuwa, kwa wadau ambao wangependa kuwasilisha maoni yao kwa maandishi wanayo nafasi ya kuwasilisha katika Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu S.L.P. 3093, Dar es Salaam iliyopo katika Jengo la Mamlaka, Barabara ya Nkrumah kabla ya tarehe 31 Agosti, 2022, na maoni yanaweza kutumwa kwa barua pepe kuititia anuani hizi: [info@latra.go.tz](mailto:info@latra.go.tz) na [dg@latra.go.tz](mailto:dg@latra.go.tz).

Hivi karibuni, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilipokea maombi kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) ikiomba ongezeko la nauli kwa asilimia 15 kwa abiria wanaotumia usafiri wa treni Tanzania Bara. LATRA itafanya mikutano mengine kwa mikoa ya Kigoma, Mwanza na Arusha ili kuwafikia wadau na kupata maoni zaidi kuhusu pendekezo la nauli hizo.



# MKURUGENZI MKUU LATRA ATOA POLE KWA MKUU WA MKOA WA SIMIYU



**M**kurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo, ametoa salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. David Kafulila ku-fuati ajali mbaya iliyotokea mkoani humo kwa magari mawili aina ya Pro-box na Wish yenyenamba za usajili T559 DGU na T 472 DWN, mtawalia, kugongana yakiwa kwenye mwendokasi na kusababisha vifo vya watu watano (5) na majeruhi kumi na mmoja (11).

Katika salamu zake, CPA Suluo ametoa pole kwa wafifa wote na kuwaombea majeruhi uponaji wa haraka.

Aidha, CPA Suluo amemshukuru Mhe. Kafulila kwa ushirikiano anaoipatia mamlaka hiyo katika udhibiti wa huduma za usafiri mkoani Simiyu na kwa kutoa zuio tarehe 13 Julai 2022

kwa magari madogo maarufu kama ‘mchomoko’ kutoa huduma za kusafirisha abiria kwa masafa marefu kwa kuwa magari hayo si salama kutoa huduma hiyo.

“Nawakumbusha wamiliki wote wa vyombo vya usafiri, magari ya abiria -mabasi, daladala, teksi, pik-ipiki maarufu kama bajaji, bodaboda na magari ya mizigo vinavyopaswa kuwa na leseni za LATRA wahakikishe wana leseni hai kabla ya kutoa huduma.

“Madereva na makondakta wanakumbushwa kuvalaa sare, kuwa nadhifu wakati wote na kuhakikisha vyombo vyao vinakidhi matakwa ya ubora na usalama,” alisema

Aidha, CPA Suluo aliwataka wamiliki wote wa vyombo vya usafiri wa

abiria na mizigo nchini kuhakikisha wana leseni hai za LATRA kuzingatia masharti ya leseni zao wanapotoa huduma. Vilevile amewaomba viongozi katika ngazi zote kushirikiana na LATRA ili kuboresha na kuhakikisha uwepo wa usafiri bora na salama kote nchini.

Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabani inaandaa oparesheni maalumu ya ukaguzi na ufuatiliaji wa vyombo vyote vya usafiri wa abiria na mizigo na itatoa adhabu kali kwa yoyote atakayekiuka masharti ya utoaji wa huduma zinazodhibitiwa.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI  
MAMILAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

LATRA

MAWASILIANO YA VIONGOZI WA LATRA

KITENGO CHA MAWASILIANO      info@latra.go.tz  
KWA UMA

0738 00 00 31

KITUO CHA KUFUATILIA  
MWENENDO WA MAGARI (VTS)      vts@latra.go.tz

0738 00 00 43

MAAFISA WAFAWIDHI WA MIKOA

MJKOA	baruapepe	NAMBA TA SIMU
TABORA	tabora@latra.go.tz	0738 00 00 42
DAR ES SALAAM	daressalaam@latra.go.tz	0738 00 00 44
PWANI	pwani@latra.go.tz	0738 00 00 46
BUKWA	rukwa@latra.go.tz	0738 00 00 47
KIGOMA	kigoma@latra.go.tz	0738 00 00 48
SHINYANGA	shinyanga@latra.go.tz	0738 00 00 49
BUVUMA	ruvuma@latra.go.tz	0738 00 00 50
KAGERA	kagera@latra.go.tz	0738 00 00 51
MANYARA	manyara@latra.go.tz	0738 00 00 52
MOROGORO	morogoro@latra.go.tz	0738 00 00 54
SIMIYU	simiyu@latra.go.tz	0738 00 00 55
NJOMBE	njombe@latra.go.tz	0738 00 00 56
ARUSHA	arusha@latra.go.tz	0738 00 00 57
MARA	mara@latra.go.tz	0738 00 00 58
SONGWE	songwe@latra.go.tz	0738 00 00 59
LINDI	lindi@latra.go.tz	0738 00 00 60
KATAVI	katavi@latra.go.tz	0738 00 00 61
SINGIDA	singida@latra.go.tz	0738 00 00 62
MBEYA	mbeya@latra.go.tz	0738 00 00 63
TANGA	tanga@latra.go.tz	0738 00 00 64
MWANZA	mwanza@latra.go.tz	0738 00 00 65
KILIMANJARO	kilimanjaro@latra.go.tz	0738 00 00 66
IRINGA	iringa@latra.go.tz	0738 00 00 67
MTWARA	mtwara@latra.go.tz	0738 00 00 68
DODOMA	dodoma@latra.go.tz	0738 00 00 69
GEITA	geita@latra.go.tz	0738 00 00 70

PIGA SIMU BURE 0800110019 SIKU ZOTE SAH 24



[www.latra.go.tz](http://www.latra.go.tz) [info@latra.go.tz](mailto:info@latra.go.tz)



**Jarida hili limeandaliwa Kitengo cha  
Uhusiano na Mawasiliano cha Mamlaka ya  
Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kikiongozwa  
na Bodi ya Wahariri**

**MWENYEKITI**  
**CPA Habibu Suluo**

**MHARIRI MKUU**  
**Samuel Keenja**

**WAHARIRI WASAIDIZI**  
**Salum Pazzy**  
**Abdallah Mhagama**

**MWANDISHI**  
**Mambwana Jumbe**  
**MSANIFU PICHA**  
**Ibrahim Said**

**MPIGA PICHA**  
**Deusdedity Masemba**

**MSANIFU JARIDA**  
**Deusdedity Masemba**